**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR -TAMISEMI)**

**MKOA WA SIMIYU**

Shule ya Sekondari Kanadi
S.L.P. 473,
Bariadi
Tarehe 30.03.2022

Namba za Simu
Mkuu wa Shule +255783 258 400/+255676 371 881
Makamu Mkuu wa Shule +255717303 255/+255688 431 814

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023**

Ninafurahi kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022/2023 na unatakiwa kufika shuleni tarehe **____________** bila kuchelewa.

Umepangiwa tahasusi ya **_________________**, Shule ipo umbali wa kilometa 37 kutoka mjini Bariadi kuelekea Mashariki na ipo umbali wa km 38 kutoka makao makuu ya mkoa na kiasi cha km 13 kutoka makao makuu ya wilaya ya Itilima yaani Lagangabilili.Kutoka kituo cha mabasi mjini Bariadi panda mabasi madogo yaani Hiace yaendayo Migato kupitia Nanga kwa nauli ya TSH 5000/= au Bodaboda kwa nauli ya TSH. 12,000/=. Muhula wa masomo unaanza tarehe…………………. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………………. Mwisho wa kuripoti ni wiki mbili baada ya shule kufunguliwa.

## MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE

### 1. SARE YA DARASANI

***(a) SARE YA DARASANI***

1. Suruali mbili DARK BLUU (zenye marinda mawili kila upande) ISIWE MODAL
2. Mashati mawili meupe mikono mirefu zisiwe na bega za kijeshi
3. Sweta ya bluu.
4. Tai dark bluu ndefu
5. Viatu vya ngozi nyeusi visivyo chongoka na vyenye soli na visigino vifupi visivyozidi inchi moja naisiwe buti . Viwe vya kamba
6. Soksi jozi mbili (rangi nyeusi).
7. Mkanda mweusi wa ngozi

***(b) SARE YA KAZI ZA NJE***

i) Baada ya masomo (wakati wa kazi za nje na kushindia sare inayovaliwa ni suruali kijivu yenye nembo ya shule na T-Shirt ya kijivu
ii) Viatu vya raba rangi yoyote.
NB: **Usije na nguo za nyumbani wala simu au laini ya simu**

***(c) SARE YA MICHEZO***

Shule inasisitiza michezo kwa afya na makuzi bora. Hivyo uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili hiyo:
1. Bukta mbili rangi ya bluu na tshirt nyekundu
2. Viatu vya raba vya kuchezea
NB: Unaweza ukatumia T-shirt ya kushindia kwa ajili ya michezo pia, lakini ni muhimu kuzingatia usafi

## 2. MALAZI

Shule inatoa kitanda tu kwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga moja kwa moja. Kwa hiyo uje na:

(i) Shuka mbili rangi ya Pink iliyokolea mto na foronya mbili za Pink
(ii) Kanda mbili jozi moja kwa ajili ya kuogea
(iii) Uje na mswaki, dawa ya meno, sabuni za kufulia na kuogea za kutosha muhula mzima
(iv) Uje na chandarua kwa ajili ya mbu na ndoo mbili, moja kwa ajili ya kuogea na moja kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
(vi) godoro la futi sita kwa mbili na nusu
(v) Uje na toilet paper kwa matumizi yako.

## 3. MAHITAJI YA TAALUMA

a) **Rimu 1** kwa mwaka A4 aina ya ROTATRIM , WATER MARK,DOUBLE A, NOPATOP au MONDI pekee
b) Result slip ya kidato cha nne (CSEE) Nakala
c) Cheti cha kuzaliwa Nakala

## 4. MAHITAJI YA DARASANI

i. Madaftari 05 (Counter Book)
ii. Kalamu/Penseli za kutosha
iii. Mkebe wa hisabati (Mathematical Set)
iv. Kwa mwanafunzi wa PCB alete dissection kit kwa ajili ya kujifunzia
v. Scientific calculator kwa wanafunzi wa PCB na PCM.
Vi .Aje na koti la Maabara “Lab Coat’’ Jeupe.

## 5. VIFAA VYA KULIA CHAKULA

Shule haina vyombo vya kulia, hivyo uje na sahani, bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya kuchukuliachakula na kulia.

## 6. FEDHA

Malipo yote yafanyike kupitia Akaunti Na. 30501100019 Kanadi Revenue Collection Account NMB-Bariadi. Mwanafunzi hatapokelewa shuleni akifika bila kuwa na **Bank Pay-InSlip** ya malipo hayo. Mwanafunzi alipe michango ifuatayo;

Karo ya shule Sh.35,000/= kwa Muhula au Sh.70,000 kwa mwaka

Michango mingine ni;
1. Mlinzi na wapishi Tsh 30,000/=
2. Taaluma Tsh 20,000/=
3. Ukarabati 15,000/=
4. Tahadhari 5,000/=
5. Kitambulisho Tsh 6,000/=
6. Nembo ya Shule Tsh 2,000/=
7. Matibabu Tsh 10,000/=
8 Uje na fedha kwa ajili ya matumizi yako binafsi, kama kununua vifaa vya kujisomea, usafi nakadhalika.
N.B: Malipo yanaweza kufanyika kwenye Tawi lolote la NMB.

Tafadhari Uje na Vifaa vya Kazi vifuatavyo:-

(i) Ndoo ya plastiki ujazo wa lita 20 moja (01),
(ii) jembe lenye mpini moja (01),
(iii) Fyekeo moja,
(iv) dekio (mop) aina ya pusher moja
(v) Fagio la chelewa moja(01) na soft broom moja (01)

**7. URAIA:**

unatakiwa kuthibitisha kuwa wewe ni raia wa Tanzania au mkimbizi anayetambulika na Serikali ya Tanzania. Njoo na uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Wilaya yako au cheti chako cha kuzaliwa.

9. Utajigharamia mwenyewe safari zote za kuja shuleni na kurudi likizo

10. Pamoja na maelekezo haya ya kujiunga naambatanisha Fomu zifuatazo

i. Fomu ya kukubali kuandikishwa na ahadi ya utii. Ijazwe na kuletwa shuleni kwa Mwalimu Mwandamizi Malezi na Utamaduni.
ii. Fomu ya kuomba kupimwa afya
iii. Orodha ya vitabu na vifaa muhimu vya kununua

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII, USAFI na TABIA NJEMA kwa ujumla Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri Kwa heshima na tabia kauli na vitendo hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri

2. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.

3. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi

(a) Kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya.
(b) Kufuga kucha na nywele
(c) Kufuga ndevu
(d) Kunyoa kipara
(e) Kumpiga mwenzake
(f) Kutukana
(g) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Heleni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali, Kofia, Kanzu, Vilemba, Suruali fupi Kwa kuwa Shule hii ni ya Serikali.
(h) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
(i) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule
(j) Kuvaa suruali chini ya kiuno
(k) Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model

4. Mwanafunzi atasimama mstari wakati wa kupata huduma

5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali

6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu Kwa wengine anapokuwa Darasani Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi nk

7. Mwanafunzi LAZIMA awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.Hivyo Mwanafunzi:-

A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.

B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa

C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa

D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi , kupandisha Bendera ya Taifa, Mikutano ya nyumba, Mikutano ya darasa na Maabara za shule.

8. Ni LAZIMA mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na KITAMBULISHO kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule.

9. Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu kwenda Posta, Kanisani,Msikitini,Benki ,Hosipitali,likizo au kwa shughuli yoyote itayokulamzimu kwenda nje ya shule.

10. Ni LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali(pass) cha maandishi.

11. Mwanafunzi lazima ahudhurie prep inayoanza saa 1.30 jioni na awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa (lights out) saa 5: 00 usiku.

12. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia chakula bwenini, wala kutumia electrical heater au jiko la aina yoyote 13. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhutasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.

14. USAFI:

Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi Kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.

15. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za **shule ya sekondari Kanadi** muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati lake. Mavazi ya nyumbani Hayaruhusiwi kabisa.

16. Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki **simu** au **sehemu ya simu kama laini, Charger earphone, Ipadi** nk. 17. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.

18. MAENEO YASIYORUHUSIWA:

Mwanafunzi haruhusiwi kufika/kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu:

a. Ofisi za shule.

b. Kwenye disko, ngoma , mziki au kwenye sherehe yoyote ndani na nje ya shule
c. Maabara. Baa,kilabuni au mahali popote panapouzwa pombe au vileo vingine
d. Nyumba za wageni ( Guest House)
e. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi kuuza, kutumia au kubeba pombe, bangi au vileo vingine.
f. Nyumba za watumishi/walimu

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI AU KUSIMAMISHWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na ulawiti.
3. Ulevi wa aina yoyote.
4. Utumiaji wa madawa ya kulevya km vile uvutaji wa Bangi,Cocaine ,Mirungi,Kubeli nk.
5. Uvutaji wa sigara au Bangi
6. Makosa ya jinai
7. Kuoa au kuolewa
8. Kuharibu Kwa makusudi Mali ya umma.
9. Kupigana au kumpiga mwingine.
10. Kudharau Bendera ya Taifa
11. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule

12. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma Kwa namna yoyote
13. Kutoa lugha ya matusi
14. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
15. Kutohudhuria vipindi
16. Ubakaji.
17. Kuwa na simu ya mkononi.

±

MAMBO MENGINE YA MUHIMU ANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

• Medical examination formu ambayo itajazwa na mganga wa Hospitali ya Serikali mara tu atakapowasili shuleni na kuikabidhi.

• Fomu ya Melezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshirki katika migomo ,fujo na makosa ya jinai

• Fomu ya mzazi kukiri kukubalina na sheria ,kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

NB:Asipo kamilisha maagizo haya hatapokelewa wala kusajiliwa shuleni

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI KANADI

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE

(Ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa mkuu wa shule)

1. Jina kamili……………………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa…………………..Wilaya………………………………….

3. Taifa………………………………………………….

4.Shule unayotoka………………………………………………

AHADI ZA MWANAFUNZI

(a) Naahidi kutii na kuzifuata sheria zote za shule kama zilivyoambatanishwa.

(b) Naahidi kuwa sitathubutu kuanzisha wala kushiriki katika mgomo wa aina yoyote ile hapa shuleni.

(c) Naahidi kuwa nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa mbele ya uongozi wa shule endapo nitasikia tetesi au taarifa ya kuaminika juu ya jambo lolote linaloashiria kuleta vurugu au ukosefu wa

amani shuleni. Pia nitafuata utaratibu wa kumaliza matatizo shuleni kwa kutumia vikao halali.

(d) Naahidi kutotoka nje ya eneo la shule kwa kipindi chote cha kuwepo kwangu hapa shuleni na kutokukaribisha mgeni yeyote kukaa ama kulala bwenini bila idhini ya uongozi wa shule.

(e) Naahidi kuwa sitavaa suruali za kubana (Vimodo), kofia pamoja na nguo ambazo si sare ya shule (nguo za nyumbani).

(f) Vile vile naahidi nitakula chakula kilichoandaliwa siku husika kutokana na utarabitu wa shule.

(g) Naahidi na kuamini kwamba dhumuni langu kuwa hapa shuleni ni kupata elimu na si vinginevyo.

(h) Naahidi nitafanya mazoezi yote, majaribio yote, mitihani yote ya nje na ndani (Mock and National Examination).

(i) Ninaahidi kuwa nitashiriki bila kukosa masomo ya usiku (Night Preparation) kufuatana na ratiba yashule darasani kwangu.

Mimi ………………………………………………Kidato cha ……..… Baada ya kusoma kwa makini na kuelewa sheria za shule na ahadi za mwanafunzi zilizowekwa Na Uongozi wa shule. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu pamoja na Mkuu wa Shule kuwa nitazitii; kuzingatia; kutekeleza na kufuata sheria zote za shule na kwamba nikizivunja sheria za shule nijihesabu nimejifuta shule mwenyewe.

Jina kamili na sahihi ya mwanafunzi………………………………..……Tarehe………………… Jina kamili na sahihi ya Mzazi/mlezi wangu…………………..…………………. Tarehe……… Namba ya simu ya mzazi/mlezi …………………………

Taja jina la mtu wa karibu ambaye shule inaweza kuwasiliana nae kwa jambo lolote iwapo mzazi/mlezi akikosekana……………………………….Anwani………… namba yake ya simu……………………….

Jina na sahihi y3a Mkuu wa Shule …………………………….. Tarehe ……………………..

VITABU ANAVYOPASWA KUWA NAVYO MWANAFUNZI

| MATHEMATICS | ENGLISH | GEOGRAPHY | BIOLOGY | CHEMISTRY | PHYSICS |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Advanced maths by L.K.Turner I & II, 2. Advanced maths by C.J.Tranter,<br>3.Advanced maths by L.K.Shayo,<br>4. Advanced maths by Backhouse Vol.I & II.<br>5.Advanced maths Vol.I & II<br>6.Understanding Mathematics<br>7.Electronic Calculator (Scientific Function 1991) | 1. Advanced literature by Nyambari Nyangwine<br>2. The real English Advanced Level by Dr.Michael Kadeghe<br>3. New Advanced Level English by Charles .E. Shalua<br>4. Introduction of Phonology by Gimson<br>5. A University Grammar of English<br>6. A complete English course for Form V & VI by Dr.Michael Kadeghe<br>7. Oxford Advanced learners Dictionary | 1. A practical Guide to Statistical Maps and Diagrams by H.C.Truran<br>2. Practical Geography for Africa by J.M.Pritchard<br>3. Principles of Physical Geography by F.J.Monkhouse<br>4. Human and Economic Geography by G.C.Leong and G.C. Morgan<br>5. Map Reading by Zisti Kamili<br>6. Photo Interpretation by kura<br>7. Physical Geography ALevel by D.T .Msabila<br>8. Physical Geography by R. Bunnet | 1. Biological Science by Taylor et al (Cambridge)<br>2. Advanced Biology by Sinpkins (ELBS)<br>3. Understanding Biology by Co Susan Trole<br>4. Understanding Biology by Nelson Thornes | 1. A level chemistry by (E.N.Ramsden)<br>2. Advanced level Inorganic Chemistry Part I & II 3. Organic Chemistry Part A & B by Tanzania Publishing House 4. Physical Chemistry by Mzumbe 5. Advanced Level Chemistry by Ramsden | 1. Advanced Level Physics by (M.Nelkon & P.Parker),<br>2.Concise "A"Level Physics By (Arwahyses),<br>3.Physics by (Tom Duncan),<br>4.New Intermediate Physics, 5.Rodger Muncuster by (Rodger Muncuster),<br>6.Calculation of Advanced Level Physics by (Tllower and J.F.Rounce). |
| **HISTORY** | **KISWAHILI** | | | | |
| 1.Advanced level History for form Five and SIX by Oxford<br>2.Advanced level History paper 1&2 by Z.Kamili<br>3.The Evolving world by Denis Ngalula | 1.SAMAKIS A na SAMAKISA vya Masmaba na Wenzake<br>2.Kiswahili Kidato cha Tano na Sita by Oxford<br>3.Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili 2 | | | | |

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KANADI

ZACHARIA ANGELO NOGU

MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
KANADI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 473-BARIADI

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART 'A'

TO THE MEDICAL OFFICER                                        FROM

……………………………                                        ………………………

………………………………                                        ………………………..

Mr.……………………………………………………(Name in full)

Please examine the above named as to his physical and mental fitness for a full – time student. The examination should include the following categories (I – III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect

I (a) Eyesight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Limbs
(e) Venereal Diseases
(f) Leprosy
(g) Epilepsy
(h) TB

II Neuroses

III Other serious diseases

Date…………………………………Signature………………………………

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above – named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I (a) Eyesight……………………
(b) Hearing…………………….
(c) Speech…………………….
(d) Limbs………………………
(e) Venereal Diseases…………………
(f) Leprosy……………………………...
(g) TB …………………………………..

II Neuroses……………………………………………………………………….................

III Other serious diseases …………………………………………………………………..

Date…………………………………………Signature…………………………….........
Station……………………………………... Designation………………………………